

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَكِلُوا الصَّدِيقَاتِ لِيَسْتَخْفَتُنَّهُنَّ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَنْتُخْلُفُ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُسْكَنَنَّ لَهُنْ دِيْنُهُنَّ الَّذِي أَرْتَقُنَّ لَهُنْ وَلَيُسْبِئَنَّهُنَّ مِنْ بَعْدِ حَرْقَهِنَّ أَنَّا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْكُوْنُ فِي شَيْءٍ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّاغِنُونَ



Jumanne, 16 Rajab 1444 H

07/02/2023 M

Na: HTS 1444 / 30

Taarifa kwa Vyombo vyahabari

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir / Wilayah ya Sudan Wakutana na Rais wa Baraza la Fiqh ya Kiislamu (Imetafsiriwa)

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir / Wilayah ya Sudan, ukiongozwa na Ustadh Ibrahim Othman (Abu Khalil) - Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir katika Wilaya ya Sudan, akifuatana na Ustadh Abdullah Hussain - Mratibu wa Kamati Kuu ya Mawasiliano ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah ya Sudan, na Ustadh Khalid Al Noor - Mwanachama wa Hizb ut Tahrir, walikutana na Baraza la Fiqh ya Kiislamu jijini Khartoum, Dkt. Abd Al-Rahim Adam Muhammad - Rais wa Baraza, na Mhandisi Al-Zubair Muhammad Ali - Katibu Mkuu wa Uimarishaji wa Fikra katika Baraza. Hii ikiwa ndani ya wigo wa mikutano ya Hizb ut Tahrir/Wilayah ya Sudan na viongozi wa jamii, wasomi, wanasiasa na wengineo, kama sehemu ya kampeni ya hizb ya kutokomeza miadarati.

Baada ya kuukaribisha ujumbe huo, mkuu wa ujumbe huo, Ustadh Abu Khalil, alizungumzia madhumuni ya mkutano huo, na kwamba uliingia ndani ya wigo wa kampeni ya Hizb iliyozinduliwa katika Shirika la Habari la Sudan (SUNA) kupambana na miadarati, akionyesha kuwa miadarati ni njia mojawapo ya vita vya kisasa, ambavyo ni vita vya kizazi cha tano, na kwamba tangu mwaka 2013, dawa za kulevyta zimekuwa zikfurika Sudan, ili kuharibu fikra za vijana wanaotegemewa kwa mabadiliko ya kweli, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

Abu Khalil pia alionyesha ukosefu wa umakini wa serikali katika kupambana na miadarati. Badala yake, mkuu wa Baraza Kuu, Al-Burhan, anapeana mikono na mhalifu muuji Cohen, waziri wa mambo ya nje wa umbile la Kiyahudi, akiua kuwa dola ya Kiyahudi inahusika katika kuishheheni Sudan kwa dawa za kulevyta, na kwa hivyo haipasi kuitegemea serikali hii ili kuondoa dawa za kulevyta, bali ni lazima tufanye kazi ya kusimamisha dola ya Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, ili vijana na jamii ihfadhiwe, kuitia kuondoa madawa ya kulevyta na maovu yote mara moja.

Kisha Dkt. Abd Al-Rahim akazungumza, akisema: Nyinyi pekee ndio mnaojua dori ya baraza hili, na kwa hilo tunawashukuru kwa ziara hii, na kwa juhudini mnazozifanya katika suala hili, kuashiria kwamba wao pia wana mipango katika mapambano dhidi ya miadarati. Kisha akampa nafasi Ndugu Al-Zubayr - Katibu Mkuu wa Uimarishaji Fikra katika Baraza, ambaye alieleza kwa kina mipango wanayoifanya.

Kwa kumalizia, mkuu wa Baraza la Fiqh ya Kiislamu alikubali kwamba kukabiliana na tishio hili la Magharibi kunaweza tu kufanywa na dola yenye nguvu, ambayo ni Dola ya Khilafah. Ndugu Abdullah Hussain aliwasilisha baadhi ya machapisho yanayohusiana na suala la madawa ya kulevyta yaliyotolewa na hizb, pamoa na matoleo ya Jarida la kila wiki la Ar-Raya linalotolewa na Hizb ut Tahrir.

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Sudan**